Jumuiko la Maliasili Tanzania
Tanzania Natural Resource Forum

Makala ya Kisera

Muhtasari wa Utatuzi wa Mgogoro wa Ardhi Loliondo

Mwezi wa Pili 2011

Muhtasari

Kwa miaka sasa, kumekuwa na mgogogro Loliondo kuhusiana na na matumizi ya ardhi na rasilimali za asili. Mgogoro ni changamani, ukiwahusisha wadau wengi, lakini chanzo cha tatizo ni bayana - udhibiti dhaifu wa ardhi. Mgogoro ulifikia kilele Julai 2009, ukisababisha kuunguzwa kwa maboma, ukiukwaji wa haki za binadamu, upotevu wa ng'ombe 50,000 na hasara nyingi kwa jamii katika eneo hili. Tangu wakati huo zaidi ya tume 15 zimefanya uchunguzi, na hata hivyo, hakuna mabadiliko wala maendeleo. Ni nini kitahitajika kuleta amani katika eneo hili bado kunahitaji mjadala. Maelezo haya mafupi hubainisha kwa muhtasari mambo muhimu yaliyojitokeza na mapendekezo ya ki-sera ambayo ni muhimu sana katika kuufikia muafaka wa haki, uadilifu na usawa. Katikati ya suala hili kuna fikra kwamba manufaa ya jamii na haki zao ni lazima kuzingatiwa, ambapo kwa kifupi kunamaanisha kwamba jamii ni lazima zisimamie udhibiti wa ardhi Loliondo.

Utangulizi

Loliondo ipo Kaskazini Magharibi mwa Mkoa wa Arusha, ikipakana na sehemu muhimu za kitalii na za kiikolojia: Hifadhi ya taifa ya Serengeti, Eneo la Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro na Ziwa Natron. Kuna vijiji vingi Loliondo, saba kati yao ni mkabala na Hifadhi ya Serengeti, ambako ardhi zao zilikuwa zikitumika kwa uwindaji, utalii wa picha, kuishi, kilimo na ufugaji. Inakadiriwa kuwa asilimia themanini (80%) ya wanajamii katika vijiji hivi ni wafugaji, wanaotegemea mifugo kwa maisha yao. Ardhi ya vijiji hivi aidha iliainishwa kuwa maeneo Tengefu ya Wanyamapori (GCA) tangu enzi za ukoloni.



Mwishoni mwa miaka ya 1980, ardhi iligwanywa kwa kuongeza uwekezaji wa kilimo, kulikohatarisha au kuathiri uhamaji wa wanyamapori na matumizi ya ardhi ya wafugaji Loliondo. Kutokana na hali hii, vijiji, mamlaka ya wilaya, Hifadhi za Taifa na Wizara ya Ardhi zilifanya kazi pamoja kuhakikisha kila mdau anapata hati miliki ili jamii ziendelee kuwa na mamlaka juu ya ardhi yao. Ili kuboresha usimamizi wa rasilimali zao, vijiji vyote vilitunga sheria ndogo ndogo na kuweka mipango ya matumizi ya ardhi. Mipango hii ya ardhi hutenga maeneo mahsusi kwa kwa matumizi tofauti ya ardhi. (mf. Kilimo, makazi, utalii,malisho wakati wa kiangazi, malisho wakati wa masika nk.). Hata hivyo,mnamo mwaka 1992 eneo tengefu la Loliondo ambalo ni eneo la uwindji wa kitalii (Loliondo GCA hunting block) lilikodishwa kwa shirika la Ortello Business Corporation (OBC) bila kushauriana na jamii. OBC wameshikilia haki za umiliki wa eneo hili pasipo kuingiliwa, tangu wakati huo. Mwingiliano wa Eneo tengefu la uwindaji chini ya OBC na ardhi ya vijiji hivi, ni chanzo kikuu cha mgogoro unaoendelea hadi sasa.

Mabadiliko ya hivi karibuni ya sheria (2010) yalifanya mwingiliano kati ya maeneo tengefu na ardhi ya vijji kuwa batili yaani kinyume cha sheria, ikiwa ni pamoja na marufuku ya matumizi eneo hilo kwa wenyeji. Kutokana na hali ilivyo basi, sasa ni muafaka kuuweka mtazamo wa chaguzi, ili mgogoro huu wa matumizi ya ardhi uweze kupatiwa suluhu.

Chaguzi za matumizi ya ardhi

Uchaguzi wa 1: Ardhi ya kijiji

Eneo lote linabaki ni Eneo la Kijiji chini ya Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Kijiji ya mwaka 1999 na chini ya sheia hizi usimamizi utazingatia kimsingi mpango wa matumizi ya ardhi katika ngazi ya kijiji na sheria ndogo ndogo za matumizi ya ardhi ya kijiji. Hivi ndivyo hali halisi ya eneo la Loliondo lilivyokuwa kwa miaka ishirini iliyopita. Matokeo muhimu kwa uchaguzi huu ni:

- *Maslahi (Livelihoods):* Maslahi ya jamii yataimarika zaidi na mashaka na matatizo kuhusiana na ardhi yatakuwa yameshughulikiwa na kutatuliwa.
- *Azimio (Resolution)*: Uchaguzi huu huimarisha amani na usalama wa muda mrefu kwa watu wa Loliondo, kwani utahakikisha ufikiaji na usimamizi wa rasilimali kwa maisha na shughuli za kiuchumi, pia kuunga mkono haki za jamii kwa ardhi yao.
- *Matumizi ya ardhi (Land Use)*: Uzalishaji wa mifugo utakuwa ndio shughuli kuu ya matumizi ya ardhi na ya kiuchumi, wakati hoja na masuala ya utalii na uwindaji yatashughulikiwa na jamii.
- *Mapato (Revenue)*: Jamii zitashiriki kwa namna nyingi katika utalii na ndizo zenye mamlaka kwa shughuli hizo. Hata hivyo, kuna uwezekano kwamba haki ya uwindaji ya OBC itabatilishwa, ambapo kutasababisha serikali na jamii kupoteza takriban dola za Marekani 819,000 kwa mwaka. Pamoja na upotevu huu, jamii zitajipatia kati ya dola 3,000,000 na 4,000,000 kutokana na kujihusisha na utalii na uzalishaji wa mifugo.
- *Uhifadhi (Conservation)*: Hakuna uthibitisho wa matukio hasi ya muda mrefu kuhusiana na idadi ya wanyamapori Loliondo, na ushahidi unaonesha kuwa wenyeji wa Loliondo hawaathiri uhamaji maarufu wa nyumbu. Upo uwezekano kuwa hifadhi wa wanyamapori utabaki kama ulivyo sasa, hususan iwapo jamii za wenyeji zitaweza kufaidi kutokana na juhudi za uhifadhi wa wanyama pori.

Chaguzi	Maisha imara ya jamii	Utatuzi matatizo	Matumizi anuwai ya ardhi	Uzalishaji mapato	Uhifadhi
Ardhi za vijiji	***	**	***	***	*
Eneo Tengefu (GCA)				*	**
Hifadhi za Jamii (WMA)	***	***	***	***	***

Jedwali 1: Hili linaonesha matokeo ya chaguzi tofauti. Nyota huwakilisha "nzuri" – nyota moja ikiwa inafaa na nyota tatu ikionesha kuwa ni bora zaidi.

Uchaguzi wa 2: Ardhi tengefu

Eneo lote, likijumuisha eneo lenye mgogoro, limeainishwa kama eneo tengefu na Sheria mpya ya Uhifadhi wa wanyama pori ya 2009. Malisho ya mifugo ya aina yoyote, Kilimo na hata makazi yatapigwa marufuku ila shughuli za uwindaji zitabaki.

- *Maslahi (Livelihoods):* Takriban watu 20,000 wataondolewa katika eneo lenye mgogoro, na uzalishaji wa mifugo katika wilaya utapungua kwa kiwango kikubwa kwa kuwa maeneo muhimu ya malisho na maji yataondolewa katika usimamizi wa vijiji na matumizi ya jamii. Hii itakuwa na athari hasi kwa maisha ya wana jamii na uchumi wa wilaya kwa ujumla.
- *Azimio (Resolution)*: Kwa kuwa jamii zitapoteza ardhi yao na maisha yao yataathirika vibaya, upo uwezekano kwamba mgogoro wa ardhi na rasilimali Loliondo utaendelea ama utaongezeka. Hali hii inaweza kusababisha kuendelea kutangazwa vibaya kimataifa, matatizo na wadau wa kimaendeleo, na migongano kati ya serikali na jamii za wenyeji.

- *Matumizi ya ardhi (Land Use):* Upo uwezekano wa OBC kupewa matumizi pekee ya eneo lote lenye mgogoro kwa ajili ya uwindaji wa kujistarehesha. Hata hivyo , eneo hili litakuwa Tengefu (GCA), hakutakuwa na aina nyingine ya utalii ama malazi ya kitalii, na shughuli za ufugaji na kilimo zitapigwa marufuku.

- *Mapato (Revenue):* Mapato kutokana na uwindaji wa OBC yataingiza takriban dola za Marekani $800,000 kwa mwaka; kuna uwezekano wa kiwango hiki kuongezeka kutokana na OBC tayari imeanza kulipa zaidi ya viwango vya soko kwa kitalu cha Loliondo. Hata hivyo, aina nyingine zote za utalii zitasimamishwa na kwa kuondosha kabisa shughuli za ufugaji katika eneo lenye mgogoro, hasara kwa mwaka zinakadiriwa kuwa kati ya dola 3,000,000 hadi 4,000,000. Hakutakuwepo basi vichocheo au hamasa za kiuchumi kwa jamii za wenyeji kuhifadhi wanyamapori nje ya eneo tengefu (GCA), ikisababisha uwezekano wa athari hasi kwa uhamaji wa kila mwaka.



Vyanzo: Ripoti ya TNRF "Integrating Pastoralist Livelihoods and Wildlife Conservation." Taarifa hapo juu ina misingi katika taswira zifuatazo za ukusanyaji mapato: mapato kutoka uwindaji hufikia $819,000 kwa mwaka; Utalii $360,000 kwa mwaka, ila haijaendelezwa kutokana na mgogoro; Utalii (au uwezo wa Loliondo) ukizingatia mapato toka SNP kufikia $2,100,000 kwa mwaka; Mauzo ya mifugo Loliondo kufikia $3,015,400 kwa mwaka. Eneo Tengefu (GCA) litapata mapato toka uwindaji pekee, Hifadhi za Jamii (WMA) na Ardhi za vijiji zaweza kukusanya mapatp toka utalii na mifugo. (Upo uwezekano yasipatikane kwa winai toka uwindaii wa OBC)

- *Uhifadhi (Conservation):* Faida za uhifadhi wa wanyamapori zitapatikana kuokana na uchaguzi huu kama njia kuu ya matumizi ya ardhi. Hata hivyo, kukataza mifugo yote katika Eneo Tengefu (GCA) kunaweza kusiwe na manufaa kamili kwa wanyamapori, kwani utafiti mwingi umebainisha kwamba ulishaji wa mara kwa mara wa mifugo hufaidi aina nyingi ama spishi anuwai za wanyama pori kwa kupunguza urefu wingi wa malisho na kuongeza ubora wa malisho. Athari za kuongeza idadi ya mifugo nje ya maeneo tengefu, zaweza kuwa na athari kwa wanyamapori na uhamaji wa kila mwaka, hasa katika miaka ya ukame.

Uchaguzi na. 3: Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori - Wildlife Management Area (WMA's)

Maeneo ya Hifadhi ya Wanayama (WMA's) yapo kwenye ardhi za vijiji kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za asili ambapo jamii wenyeji hupewa kiwango cha haki za matumizi ya wanyamapori, ambazo zitawezesha jamii kufaidika kutokana na uwindaji na utalii. Matumizi mengine ya ardhi kama Kilimo, makazi na ufugaji yanaweza kuendelea kwa kadri ya makubaliano ya mipango iliyowekwa.

- *Maslahi (Livelihoods)*: Maeneo ya hifadhi wanyamapori vjijini (WMA) yangeliweka uwiano wa faida kati ya vijiji /wafugaji na utalii ama uwekezji wa uwindaji na faida za uhifadhi wanyamapori katika mfumo rasmi. Uhifadhi wa jamii (WMA) ungeliruhusu matumizi yote ya ardhi yanayoendelea sasa, ambayo yangelisaidia kuboresha maisha ya wenyeji kwa uchumi utokanao na vyanzo anuwai.

- *Azimio (Resolution)*: Chini ya WMA, ardhi ingebaki kuwa ya kijiji ikisimamiwa na kumilikiwa na viijiji. Hii ingeliridhisha shauku mojawapo ya jamii nahivyo basi kuwa ni muundo unaofaa katika utatuzi wa matatizo na kuondosha uwezekano wa kutokea migogoro ya matumizi ya ardhi katika eneo hilo katika siku za baadae. Hata hivyo, kwa vile OBC ilihusika katika mgogoro, hakuna uwezekano wa jamii kuwaongezea haki za uwindaji.

Mabadiliko kuwa Eneo Tengefu (GCA) – hii humaanisha nini na ni kwa nini ni lazima itafutiwe suluhu!

Tarafa za Loliondo na Sale kwa pamoja zina sifa bainifu za maeneo ya vijiji kuingiliana au kufunikwa na GCA. Hata hivyo, mnamo 2009, mabdiliko ya sheria ya wanayamapori, imebainisha kuwa matumizi yoyote ya ardhi yahusianayo na shughuli za kiuchumi za binadamu ama makazi haziwezi kufanyika katika GCA. Mabadiliko haya husababisha masuala hatari kwa Loliondo; hata hivyo siyo Loliondo tu inayoathirika kwa sheria hiyo. Wilaya za Longido, Monduli, Simanjiro nazo zina mwingiliano kati ya Vijiji na GCA.

- *Matumizi ya ardhi (Land Use)*: WMA ungeliruhusu matumizi nyumbulifu ya ardhi kwa njia shirikishi, ambapo malisho na maji yanweza kufikiwa, wakati huo huo uwindaji na aina anuwai za utalii zinaweza kuanzishwa pia.

- *Mapato (Revenue)*: Chini ya WMA, shughuli mbalimbali za matumizi ya pamoja ya ardhi zinaweza kutekelezwa ambapo zinaweza kuongeza shughuli za kuinua uchumi katika eneo hilo. Makadirio ya utalii na ufugaji yanaweza kufikia dola 5,000,000 (kwa mujibu wa uwezo wa mapato toka Hifaadhi ya Serengeti).

- *Uhifadhi (Conservation)*: WMA ingelikuwa bora kwa faida za uhifadhi, kwani ingelihakikisha ulinzi na kuweka hadhi ya uhifadhi rasmi katika maeneo muhimu ya makazi ya wanyamapori na mapito katika eneo hili. Faida za jamii kutokana na WMA kutatoa motisha za nguvu kuhifadhi wanyamapori na makazi yao hata nje ya WMA ikidumisha uwezekano wa uwepo wa uhamaji wa nyumbu kwa muda mrefu katika eneo hili.

Mustakabali wa Loliondo

Wadau wote wanaweza kukubali kuwa Loliondo haiwezi kubaki hivi kwenye migogoro ya kudumu na hofu. Mambo mengi yako hatarini, wengi wanahusika, na bila utatuzi uharibifu zaidi utatokea. Zaidi ya hayo, mabadiliko ya maana au tafsiri ya Eneo Tengefu (GCA) kunaongeza umuhimu wa kutatua tatizo la matumizi ya ardhi Loliondo. Tathmini ya chaguzi zilizobainishwa hapo juu yaweza kuweka bayana namana inayofaa kwa maamuzi ya baadaye.

Ujumbe muhimu

- Mgogoro wa ardhi Loliondo ni lazima utatuliwe ili amani irudi kwenye eneo hilo. Kwanza, ili uwepo usuluhisho wa kudumu , umiliki wa sasa wa ardhi na haki za ardhi za jamii Loliondo hazina budi kutambuliwa na kuheshimiwa.

- Uzalishaji mifugo ni namna muhimu ya matumizi ya ardhi yenye tija kiuchumi Loliondo, kufikia dola $3,000,000 kwa mwaka. Chaguzi za matumizi ya ardhi zizingatie na kuupa kipaumbele ufugaji kwa ajili ya umuhimu wake kiuchumi.

- Kuna chaguzi tatu kuu za umiliki ardhi kwa namana ya kwenda mbele – maeneo tengefu; Ardhi ya kijiji; WMA au hifadhi ya jamii. Na ili kuhakikikisha kuwa mgogoro umesuluhishwa moja kwa moja, uchaguzi kati ya chaguzi uwe kwa jamii.

- Takriban watu 20,000 wanaishi katika eneo lenye mgogoro, na maisha yao yanategemea sana ufugaji. Iwapo eneo la mgogoro litakuwa Eneo tengefu (GCA),watu hawa wataondolewa kutoka ardhi yao na mgogoro utabaki haujatatuliwa kwani maisha yao yataathirika vibaya.

- Kati ya chaguzi za umiliki ardhi, WMA, na ardhi ya kijiji huzipa jamii haki za kudumu za ardhi na usimamizi wa rasilimali. Katika ardhi yan kijiji jamii huwa na haki zaidi kwa rasilimali asili, isipokuwa wanymapori. Mipango ya matumizi ya ardhi huwawezesha wanajamii kusimamia rasilimali kwa njia endelevu.

- Uchaguzi wa WMA hutoa uwiano sawa kati ya manufaa tofauti. Ardhi hubaki ni ya kijiji, bali matumizi anuwai ya ardhi huweza kuwepo kama vile uwindaji, utalii, Kilimo, na ufugaji. Kuchagua WMA kunaweza kuinua uhifadhi wa wanyamapori Loliondo ambao utawaletea faida jamii wenyeji.

Kuhusiana na taarifa hii: Mutasari huu unatokana na ripoti (“Integrating Pastoralist Livelihoods and Wildlife Conservation? Options for Land Use and Conflict Resolution in Loliondo, Division, in Ngorongoro District.”) Takwimu zote na rejea zinapatikana katika ripoti hiyo. www.tnrf.org.

©Copyright Tanzania Natural Resource Forum 2011